# Wajasiriamali wawekewa mikakati bidhaa bora

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

# MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. Na. 11, Jumanne Januari 28, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100

## WENGI WASUBIRI KUMSIKIA...

# Rais Samia kuishusha pumzi Afrika



- Hii ni katika hotuba yake kwenye mkutano wa Mission 300 unaofanyika Dar
- Amechangia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Tanzania kimataifa
- Viongozi wote wa afrika watakaa tayari kumsikia

## BITEKO: AFRIKA IMEPIGA HATUA NISHATI

# Rais Samia kuishusha pumzi Afrika

NA MWANDISHI WETU

**WAKATI Mkutano wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ujulikanao kama Mission 300, ukiwa umeanza jana, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa 'kuishusha pumzi' Afrika pale atakapounguruma kwenye mkutano huo leo**

Rais Dkt. Samia ambaye amejitwisha zigo la kuipigania nishati safi, anatarajiwa kusikilizwa na wengi haswa kina mama wa Afrika, ambao wengi wana matarajio makubwa naye ya kuwasemea juu ya adha wanazopata kutokana na ukosefu wa nishati safi.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia amevunja na kuandika rekodi ya aina yake kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Nchi ambao wakuu wake wamethibitisha kushiriki ni Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon. Wakati akizungumzia kwa kina mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt.Doto Biteko alisema, utakuwa ni fursa kubwa sana kwa Watanzania.

"Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania kimataifa, hii imepeleka taasisi za kimataifa, kampuni na wawekezaji kuona Tanzania kuwa ni sehemu sahihi ya kufanya biashara na uwekezaji na mfano halisi ni Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika kuichagua Tanzania kufanya mkutano huu mkubwa wa kimataifa utakahudhuriwa viongozi kitoka nchi 54 barani Afrika." Amesema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa, sababu nyingine kubwa ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huo ni mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwa wananchi suala linaloendana Ajenda ya mkutano huo ya kuharakisha kupeleka umeme kwa wananchi milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030 kati ya watu milioni 685 ambao bado hawana umeme.

"Taifa limepiga hatua kubwa katika Sekta ya Nishati, tunamshukuru Rais kwa msukumo mkubwa anaotoa katika Sekta ya Nishati, taifa lina umeme wa kutosha na wa ziada, uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1470 hadi megawati takriban 3,077."

Amesema upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwana ipo kwenye asilimia zaidi ya 78.

Akiongeza kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati, Dkt.Biteko amesema vijiji vyote 12,318 Tanzania sasa vimesambaziwa umeme na tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia barani Afrika mwaka jana imeonesha kuwa Tanzania iliongoza kwa kusambazia wananchi umeme vijijini .

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji ambapo katika vitongoji 64,000 nchini, vitongoji takriban 36,000 vimepelekewa umeme.

Ametaja faida za mkutano wa M300 kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuongeza fursa za kupata fedha za kuendelea miradi mbalimbali, kuongeza fursa za uwekezaji, kupata uzoefu kutoka kwa waliofanikiwa zaidi kwenye sekta ya nishati na kuongeza heshima ya nchi kimataifa.

Ameongeza kuwa faida nyingine ni kuharakisha upatikanaji umeme nchini ambapo kiasi cha wananchi watakaounganishiwa umeme kupitia M300 ni milioni 8.3 ifikapo 2030 na hivyo kuifanya Tanzania kuunganisha wateja milioni 13.5 kufikia 2030 Kutoka milioni 5.2 ya sasa.

# Biteko: Afrika imepiga hatua nishati

NA MWANDISHI WETU

**NCHI za Afrika zimeelezwa kupiga hatua katika suala zima la upatikanaji nishati ya umeme toka nyingi kati ya hizo zipte uhuru miaka ya 1960.**

Akisema hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko alisema hayo jana kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika 'Mission 300' unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

"Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571.kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

"Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160."

SOMA ZAIDI UK 8&9





# Wajasiriamali wawekewa mikakati bidhaa bora

NA MWANDISHI WETU

**SERIKALI imekiri bado inaendelea na mpango wa kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amebainisha mpango wa Serikali katika kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika.

Kigahe alisema Serikali imeweka mipango kadhaa ya kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ikiwa ni pamoja na kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Hii ikiwa ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupata maeneo pamoja na majengo ya kuzalishia bidhaa zao, kuwapatia mitaji kupita Mfuko wa NEDF na nembo ya ubora wa bidhaa zao kwa miaka mitatu bila gharama.

Amesema pia kupitia SIDO, TBS na Wakala wa Vipimo (WMA) wataendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu kanuni za uzalishaji wenye tija, elimu ya utambuzi wa vifungashio na ufungashaji bora

Piaamesema SIDO kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itaendelea kuandaa na kuratibu maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuchagiza ukuaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali.

Kigahe alisema, kwa sasa SIDO imekuwa na uwezo mdogo wa kuwezesha mitaji kwa wajasiriamali ambao wamekuwa wakiongezeka kila wakati.

## SIDO yaamua 'kutembea nao'

NA MWANDISHI WETU

**KATIKA utekelezaji wa mikakati yake na hususani kwenye uwekezaji, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limeendelea kuhakikisha wajasiriamali wazalishaji wanapatiwa maeneo mazuri ya uzalishaji wa bidhaa zao.**

Lengo ni kuhakikisha bidhaa za wajasiriamali zinazozalishwa zipo kwenye ubora unaotakiwa kitaifa na kimataifa.

Takribani majengo 20 yamejengwa katika mikoa mbalimbali kutokana na uhitaji mkubwa wa wajasiriamali wazalishaji. Hivi karibuni SIDO Tanga ilifanya ufunguzi rasmi wa jengo lake lililopo mtaa wa viwanda ambapo uzalishaji wa bidhaa mbalimbali utakuwa unafanyika.

Mikoa ambayo majengo haya yamejengwa ni pamoja na Kigoma, Geita, Chato, Simiyu, Katavi n Kagera. Majengo haya yana miundo mbinu mbalimbali zikiwemo umeme, maji na barabara, hii ni kwa ajili ya kuwarahisia kupokea malighafi, kuchakata, kusindika na hatimaye kusambaza bidhaa zao.

Baadhi ya wajasiriamali katika mikoa husika watafaidika na utumiaji wa majengo haya ikiwemo upatikanaji wa eneo la uzalishaji likiwa na miundombinu yote muhimu kwa bei nafuu.



## Wawekezaji toka sasa nje waitwa

NA MWANDISHI WETU

**NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amewahakikishia wawekezaji kutoka Japani kwamba Tanzania ni mahali bora kwa biashara na uwekezaji.**

Haya yamebainishwa jana katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Japani lililofanyika katika hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Kigahe aliyekuwa mgeni rasmi, alibinisha fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana nchini, zikiwemo sekta za gesi asilia, mafuta, kilimo, na matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kwa usafirishaji wa bidhaa kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Aidha, ametoa wito kwa wawekezaji kutoka Japani kuchangamkia fursa za kipekee zilizopo katika sekta ya utalii.

Amehimiza wajumbe wa kongamano hili kutembelea vivutio vya kitalii vilivyopo nchini kama vile Zanzibar, Hifadhi ya Serengeti, Bonde la Ngorongoro, na Mlima Kilimanjaro, ambavyo vinaipa Tanzania sifa ya kuwa moja ya maeneo bora zaidi ya kitalii duniani.

Kwa upande wa Ujumbe wa Japan umeongozwa na Hisayuka Fuji Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Japan kwa ushirikiano wa Balazo Baraka Luvanda Balozi wa Tanzania nchini Japan.

Kongamano hilo limehudhuriwa na viongozi mbalimbali, wakiwemo Balozi Yasushi Misawa, Balozi wa Japan anayemaliza muda wake nchini Tanzania, Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Cosato David Chumi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Dkt. Godwill Wanga, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara, pamoja na viongozi wengine kutoka Serikali na Sekta Binafsi.

Kongamano hili limewaleta pamoja wadau wa sekta za biashara na uwekezaji kutoka Tanzania na Japani, likilenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya mataifa haya mawili.

## MAONI

# HONGERA AIIB KUIPA SAPOTI AFRIKA

JANA Rais wa Benki ya Asia Infrastructure Investment Bank (AIIB), Jin Liqun aliahidi benki hiyo itatoa Dola Bilioni 1.5 kuunga mkono upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Afrika ifikapo 2030.

Ahadi hiyo ameitoa ikiwa siku ya kwanza ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaoendelea Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaendelea ukiwa ukiwa umebeba ajenda kuu ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa wakazi wote wa bara hili.

Mkutano huo uliopewa jina la Mission 300 (M300) unaongozwa na kaulimbiu inayosema: 'Kuharakisha upatikanaji wa Nishati Afrika', ukiwa na malengo ya kujadili dhana nzima ya upatikanaji wa umeme kwa wote hususan katika nyakati ambazo viongozi wa Afrika wanasisitiza matumizi ya nishati safi na salama.

Tanzania itanufaika na mkutano huo hasa ikizingatiwa kuwa wakuu wa mataifa hayo wataidhinisha Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, ambao wakuu hao wanakubaliana kufanya mageuzi yatakayosaidia kufikia lengo la upatikanaji wa nishati kwa wote kwa njia za kuaminika, nafuu na endelevu.

Takwimu za nishati kwa Afrika zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022 asilimia 83 ya watu milioni 685 walikuwa hawajafikiwa na nishati hiyo. Kwa msingi huo, mkutano huo unadhamiria kuhimiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuingia makubaliano ili umeme uwafikie watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wenye azma ya kuwafikia watu hao milioni 300, nchi 14 zitasaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika Awamu ya Kwanza.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Tunapenda kuipongeza benki hiyo kutokana na msaada mkubwa ambao umeamua kuutoa kwa Afrika, ikiwa ni kusaidia kupatikana kwa umeme barani humu.




## FIKRA YA MJASIRIAMALI

# MKUTANO WA M-300 KUWABEBA 'WAFIA TUMBO'

NA ABDUL-LATIF ALLI

**JANA na leo mataifa yote ya Afrika yataelekeza macho yake ndani ya Tanzania wakati mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati ukiwa umebeba ajenda kuu ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa wakazi wote wa bara hili**.

Mkutano huo uliopewa jina la Mission 300 (M300) unaongozwa na kaulimbiu inayosema: 'Kuharakisha upatikanaji wa Nishati Afrika', ukiwa na malengo ya kujadili dhana nzima ya upatikanaji wa umeme kwa wote hususan katika nyakati ambazo viongozi wa Afrika wanasisitiza matumizi ya nishati safi na salama.

Tanzania itanufaika na mkutano huo hasa ikizingatiwa kuwa wakuu wa mataifa hayo wataidhinisha Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, ambao wakuu hao wanakubaliana kufanya mageuzi yatakayosaidia kufikia lengo la upatikanaji wa nishati kwa wote kwa njia za kuaminika, nafuu na endelevu.

Takwimu za nishati kwa Afrika zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022 asilimia 83 ya watu milioni 685 walikuwa hawajafikiwa na nishati hiyo. Kwa msingi huo, mkutano huo unadhamiria kuhimiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuingia makubaliano ili umeme uwafikie watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wenye azma ya kuwafikia watu hao milioni 300, nchi 14 zitasaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika Awamu ya Kwanza.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Diplomasia ya kiuchumi ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na nia yake thabiti ya kuibeba ajenda ya nishati safi, ndiyo imefanikisha ujio mkubwa wa viongozi wakuu wan chi za Afrika, ambao wanakutana jijini Dar es Salaam ili kujadili nishati safi na salama.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia anatarajiwa kuvunja na kuandika rekodi ya aina yakwe kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Kwetu tunaamini mkutano huo utatoka na majibu ya kina juu ya matatizo ya upatikanaji wa nishati hiyo kwa wakazi wa bara hili na tunawaombea wote heri kubwa, wanapokwenda kujadili na kutatua tatizo la nishati ya umeme barani Afrika.



# Ushawahi kujiuliza kwa nini kilimo?



**KILIMO kimekuwepo tangu kale za mababu zetu. Binadamu wa kwanza walipata chakula chao kwenye mazingira yanayowazunguka na kwa juhudi kama uwindaji kabla ya kuanza kulima ardhi, kupanda mazao na kufuga mifugo kama vyanzo vya lishe.**

Hii ni pamoja na nafaka, mazao ya mizizi, karanga, matunda, nyama, maziwa, na hata mayai. Kilimo kimebadilisha maisha na maisha pia yamebadilisha muundo wa kilimo.

Kwa sasa, kilimo ni muhimu sana na umuhimu huu hauwezi kupungua katika miaka ya karibuni. Maadamu watu wanaishi, ni lazima wakule na wakulima wataendelea kulima!

Nini kinafanya kilimo kuonekana muhimu zaidi? Nini hufanya wakulima kutumia muda wao mwingi mashambani; kwenye jua kali, wakivuta vumbi toka kwenye ardhi iliyokauka wakati wa maandalizi ya msimu wa mvua, kuloa wakati wa mvua za rasharasha wakijaribu kupata thamani zaidi?

Watu wengi hawajawahi kufikiri kwa nini kilimo ni muhimu sana, hata wakulima wenyewe hawajiulizi hili. Tunafanya kilimo kama desturi tu, na tukijaribu kueleza kwa nini tunafanya tunachofanya, tunashindwa kujieleza au tunaeleza bila kuwa na uhakika.

**Chakula na lishe**

Upatikanaji wa chakula na lishe ni haki ya msingi ya binadamu. Asilimia kubwa ya watu duniani hutegemea wakulima ambao utumia muda wao hata wa ziada kufanya kilimo kwa ajili ya kulisha watu hawa kuishi.

Hii inasisitizwa na malengo ya maendeleo duniani (MDGs) inayoipa kipau mbele lengo la kukabiliana na njaa

Watu wengi wanaokabiliwa na njaa duniani wanaishi katika nchi zinazoendelea za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia ya Kusini.

Sehemu kubwa ya idadi ya watu nchini bado wanakabiliwa na ukosefu wa usalama wa chakula na lishe; wengi wao wanaishi maeneo kame vijijini, maeneo yenye watu wengi na ardhi ndogo, maeone yanayopakana na miji mikubwa na miji midogo zinazokua.

Haya ni maswala mazito sana katika usalama wa chakula na lishe, na kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa watu katika maeneo haya wanapata chakula na lishe bora.

Suala la chakula na lishe ni suala la usalama wa taifa. Nchi inayoshindwa kulisha watu wake iko katika hatari ya kuhadaiwa, kuchokozwa na kufanyiwa ujanja na nchi za nje. Hii ni mazingira ngumu ya kufanya kazi na kuzalisha mali.

Lishe bora hujenga kinga thabiti ya mwili na kufukuza magonjwa. Watu wenye afya bora ni nguvu kazi imara kwa taifa. Kwa mantiki hii, wakulima ni lazima watambue kuwa hawapo tu kwa ajili ya kulima bali wana jukumu kubwa ya kufanya katika taifa.

**Mbali na lishe, chakula bora huburudisha**

Hebu fikiria ni wakati wa chakula cha mchana, na unaelekea nyumbani. Ghafla, ukiwa getini kwako unakutana na mnuzo wa harufu nzuri ya pilau. Katika siku yako ya mapumziko ya wiki, upo na marafiki zako mmekaa kijiweni mlikozoea, upo na kinywaji chako.

Ghafla mlango wa jikoni unafunguliwa kwa bahati mbaya na unakutana na harufu nzuri ya nyama ya kukaanga. Kwa hakika unapataka hamasa moja kwa moja; hamu kubwa ya kumega, kutafuta, kumeza chakula kile na utamu wake wote. Hivyo ndivyo, chakula bora kutoka kilimo bora kinavyoridhisha na kufurahisha.

**Uchumi na ajira**

Kilimo ni moja ya sekta ya uzalishaji inayosaidia kukuza uchumi wa nchi. Inatoa ajira moja kwa moja kwa asilimia 75 ya nguvu kazi na huchangia moja ya tatu (30%) ya pato la ndani la taifa (GDP). Sekta ya kilimo iliyo thabiti hupimwa kwa uchumi imara, usioyumba na usiokuwa na mfumuko wa bei.

Sekta ya kilimo inaonyesha mafanikio kwa haraka na moja kwa moja inapopokea mtaji ili kuchochea uzalishaji wa mali. Hii inaonekana kupitia ukuaji wa uchumi, kuongezeka kwa nafasi za ajira na mapato kwa vijana; wengi ambao hawajasoma, hawana ustadi au wana ujuzi na uzoefu mdogo wa kufanya kazi.

Umri wa wastani wa wakulima wadogo wadogo Tanzania ni zaidi ya miaka 60. Hata hivyo, watu wapya wanaoingia katika kilimo wanaleta mbinu mpya za kuimarisha na kubadilisha jinsi ya kufanya kilimo nchini Tanzania.

Kwa namna hiyo, vijana wengi wanaaingia katika kilimo; uzalishaji wa maziwa, kuku, kilimo cha mboga-mboga, uzalishaji wa majani ya malisho na kadhalika, wanaweka jitihada katika teknolojia ili kuboresha mchakato wa uzalishaji. Hii inawaletea faida kubwa huku wanaongeza nafasi za ajira kwa vijana wenzao.

Aidha, wanatumia mtandao na mitandao ya kijamii kuwafikia wateja moja kwa moja bila kupitia kwa madalali. Hivyo, wanasaidia mkulima kuteka dhamani yote na kupata faida yake moja kwa moja kutoka kwa mlaji bila kutumia mnyororo wa watu wengi.

# Pale unapotaka kuanzisha biashara yako

NA MWANDSHI MAALUM

**MIAKA ya hivi karibuni Serikali pamoja na wadau wengine wamekuwa na mikakati thabiti ya kuwashawishi wakulima kuweka shughuli zao katika mtazamo wa kibiashara. Waliochukua na kuufanyia kazi ushauri huo kisha kufanya shughuli za kilimo, kitaalamu kwa mtazamo wa kibiashara leo wanapata faida kubwa.**

Faida hiyo haiji kirahisi. Kuwa na wazo ni aina gani ya kilimo unayoweza kuifanya kibiashara pekee haitoshi. Huo ni mwanzo tu.

Ni lazima kukusanya au uwe na pesa kwa ajili ya kugharamia shughuli hiyo, na mwisho utakapouza bidhaa zako au huduma utakayotoa uweze kupata pesa zaidi. Hapo ndipo wazo la biashara linatekelezeka.

## Mpango wa biashara ni nini?

Unapoomba mkopo, ambapo kwa kawaida mkopeshaji ni benki na taasisi nyinginezo za fedha, utaulizwa mpango wa biashara yako unayokopea fedha hizo.

Mpango wa biashara unatoa tafsiri ya malengo yako katika mageuzi ya kibiashara. Kwa nini unafikiri malengo hayo yatafikiwa, na nini mikakati ya kuyafikia malengo hayo?

Kwa bahati mbaya wakulima wengi hawajaelimika katika kufanya shughuli zao za kilimo kibiashara na kuwa na mpango wa biashara. Bila kuwa na mpango wa biashara ni vigumu sana kuweza kumshawishi mtu au taasisi ya fedha kuwekeza katika mradi wako.

Mpango wa biashara hubadilika kulingana na ukubwa wa biashara unayolenga, utaalam utakaotumika, na ni nani walengwa katika mradi huo. Kwa ujumla mpango wa biashara unakuwa na mambo yafuatayo:

### Muhtasari

Lengo la sehemu hii ni kutoa mtazamo mzima wa biashara husika na ushirika huo, unaelezea kwa ufupi biashara husika, bidhaa au huduma zitakazojumuishwa, uchambuzi wa soko la bidhaa/huduma hizo kwa ufupi, mikakati ya kupata soko, na pia uchambuzi kwa ufupi ni jinsi gani fedha hizo zitasimamiwa kuahakikisha zinafanya shughuli lengwa.

Sehemu hii ni lazima iwe wazi na ya kueleweka ili kutoa mtizamo mzuri wa biashara unayokusudia. Ni lazima uwe wazi kabisa kuelezea lengo la fedha unazokopa/omba. Muhtasari unaotoa ni lazima kuelezea kwa uhakika kuwa biashara yako itafanikiwa.

Muda mzuri wa kuandika muhtasari ni baada ya kuandika mchanganuo wa biashara na kisha uunganishe mwanzoni mwa mpango wako wa biashara.

Wazo la biashara: Hutoa taarifa juu ya bidhaa utakazouza au huduma utakayotoa.

Mpango wa Soko: Unajumuisha mambo yote unayofanya kutafuta wateja, ni nini wanachohitaji, na namna ya kuwafikia. Sehemu hii itaelezea bidhaa na huduma zako kwa undani, pia bei za bidhaa au huduma zako, na ni wapi biashara ama ofisi yako itakapokuwa na mbinu utakazotumia kusambaza bidhaa zako.

Mfumo wa biashara: Hii inaelezea mfumo wa biashara yako kisheria, mfumo uliochagua unategemeana na faida na hasara ambazo kila sheria inazo. Uchaguzi huu unaweza kuwa wa mtu binafsi, ushirika au kampuni isiyokuwa na kikomo, au ujamaa.

Katika sehemu hii pia unatakiwa uoneshe ni kwa jinsi gani ulivyofikiria mahitaji ya kisheria na ni kwa jinsi gani umeweza kufuata katika utaratibu mzima wa kuanzisha biashara yako.

Usimamizi: Sehemu hii inajibu maswali juu ya kiwango cha taaluma na uzoefu wa wafanyakazi wako, utahitaji wafanyakazi wangapi, na ni kwa namna gani elimu na uzoefu wao utakavyosaidia katika kufanikisha kufikia malengo uliyojiwekea katika biashara yako.

Mipango ya fedha: Unahitaji kuwa na bajeti. Sehemu hii itasaidia kuweza kupangilia faida na mtiririko mzima wa fedha katika biashara yako mpya.

Hii ina maana ya fedha zinazoingia (mapato) na zinazotoka (matumizi). Ukishatengeza bajeti ni rahisi kutumia taarifa hiyo kufanya hesabu ya fedha unazohitaji kwa ajili ya kuanzisha biashara yako. Huu unaitwa mtaji, na unatakiwa kuonesha chanzo cha mtaji huo. Hii ina maana ya kuonesha ni chanzo kipi kitakachochangia asilimia flani katika fedha hizo.





# Unapotaka uwe miongoni mwa mamilionea

**WATU wengi wamenaswa kwenye mbio za panya huku wakijaribu kugundua njia halisi ya mafanikio. Lakini vipi nikikuambia si lazima iwe ngumu jinsi watu walivyoifanya? Je, ikiwa ungeweza kupata mafanikio kwa kufuata tu mazoea haya ni mafanikio ya kuwa mamilionea?**



**1.Soma**

Tabia ya kila siku ambayo nimegundua mamilionea wanashiriki kwa pamoja ni kusoma. Kwa mfano, kama wewe ni mfanyabiashara, unahitaji kusoma ili kuwa kiongozi bora na mfanyabiashara mwenye tija.

Kusoma hukusaidia kukua na kujifunza bila kwenda shule ya biashara. Wakati mamilionea wakati mwingine husoma ili kujifurahisha, wao pia hujifunza kujiboresha. Wanasoma mada kuhusu uongozi, jinsi ya kufanya, jinsi ya kujisaidia, wasifu, uhasibu wa maisha na pia kufuatilia matukio ya sasa.

**2. Anzisha Vyanzo vya Mapato**

Tabia nyingine ya mafanikio niliyoona kuhusu watu waliofanikiwa ni kwamba hawategemei chanzo kimoja cha mapato. Kila milionea ana vyanzo vingi vya mapato. Hii inawasaidia kudhibiti changamoto za kiuchumi na pia kutengeneza pesa zaidi. Wao ni waraibu wa mapato tu. Wanapata riba kutoka kwa mikopo, mapato ya kupangisha nyumbaau majengo, gawio kutoka kwa uwekezaji. Pia huzindua biashara ya kando au huendesha tovuti au kuuza bidhaa za habari.

**3. Ishi kwa Bajeti**

Milionea haamini katika bahati. Wanachukua muda kuelewa mtiririko wa pesa, mapato na gharama. Kulingana na hili, wao huweka bajeti ya kila mwezi na kushikamana nayo haswa. Kiini cha bajeti ni kupunguza gharama zisizo za lazima.

Hii itakusaidia kupata udhibiti kamili wa maisha yako ya kifedha. Bajeti inakusaidia kuepuka matumizi makubwa ili kufikia malengo yako ya kifedha.

**4. Dhibiti na Uongeze Pesa**

Elimu muhimu zaidi kwa milionea ni akili ya kifedha. Hakuna mtu anayepata uhuru wa kifedha bila kupata akili ya kifedha. Hii ndiyo sababu zaidi ya milionea, bila kujali mapato yake, kusasisha maarifa yake kuhusu mikakati ya ushuru.

Wanatafuta kila wakati kupunguza bili zao za ushuru. Njia moja wanayotumia ni kwa kuishi au kujumuisha biashara zao katika majimbo au nchi ambazo hazina ushuru wa mapato.

**5. Epuka Madeni**

Tabia nyingine inayowatenganisha mamilionea na watu wengine ni jinsi wanavyosimamia madeni. Hawaishi maisha ya kupita kiasi badala yake, wananunua tu kile wanachohitaji na wanaweza kulipia.

**6. Weka Malengo**

Haijalishi ikiwa wanaanzisha biashara, kazi, au makadirio ya kifedha wana tabia ya mafanikio ya kuweka malengo ya muda mfupi. Wanapanga malengo ya kila siku na ya wiki ili kuzalisha kasi katika kufikia malengo yao ya muda mrefu.

**7. Usijione tajiri**

Lengo si kujifanya tajiri bali kuwa na tija. Jambo la kufurahisha ni kwamba Thomas Stanley alisisitiza katika kitabu chake kwamba kwa chapa maarufu zaidi za magari, karibu asilimia 86% ni vitu vya kuchezea vya wasio mamilionea.

Ingawa wengi wanaamini kwamba watu walio na utajiri mkubwa huwa na kuendesha magari ya kigeni na ya gharama kubwa, kwa kweli watumiaji wakubwa wa magari ya bei ni watu wanaotamani kuwa mamilionea.

**8. Kumiliki au Kununua Biashara**

Inajielezea yenyewe ili kupata mafanikio na utajiri huna bidi kumiliki biashara au kununua biashara zinazofanya vizuri.

9. Epuka utajiri haraka

Milionea hushikilia subira kama fadhila muhimu. Inahitaji uvumilivu ili kuwa na mafanikio, si tu katika fedha lakini katika kila nyanja ya maisha. Ingawa inawezekana kuwa na mafanikio ya kifedha katika umri mdogo, mamilionea wengi walifikia umri wa miaka 50. Wanaishi maisha ya wastani, wanawekeza katika maisha yao ya baadaye na wanastaafu matajiri.

# Afrika ipo Dar kuikomboa Afrika

**NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.**

Dk. Biteko amesema hayo kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika 'Mission 300' unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

Naibu Waziri Mkuu amesema lengo kuu la mkutano huo kuitishwa ni kufikia lengo la kuongeza upatatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571. kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

"Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160.

"Pamoja na mafanikio makubwa ya kuzalisha umeme barani Afrika, takriban Waafrika milioni 571 bado hawana huduma ya umeme. Mkutano huu umeitishwa rasmi kwa lengo la kujadili namna ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Natoa shukrani za dhati kwa waandaaji wenza wa Mkutano huu ikiwemo: Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Rockefeller Foundation; Sustainable Energy for All (SEforALL), na The Global Energy Alliance for People and Planet (GEAPP) kwa ushirikiano uliowezesha kufanyika kwa Mkutano huu.

"Uwepo wenu, mawazo na utaalamu wenu ndiyo vitakavyofanikisha Mkutano huu. Natarajia majadiliano yenye tija na tushirikiane katika kuunda mustakabali wa nishati barani Afrika.

"Natarajia mkutano huu utakuwa ni hatua muhimu katika kufanikisha lengo letu la upatikanaji wa umeme kwa wote.

"Katika mkutano huu, Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia, watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.

"Maazimio ya Nishati ya Kitaifa yaliyotayarishwa na nchi 14 zitakazokuwa za majaribio yatatoa mfumo wa utekelezaji wa hatua zilizoratibiwa ili kufungua uwekezaji zaidi kutoka kwa serikali, wabia wa maendeleo, mashirika ya misaada na sekta binafsi katika kufanikisha malengo ya upatikanaji wa nishati.

"Kupitia uhamasishaji wa rasilimali na utaalamu katika kuharakisha juhudi za kupeleka umeme barani Afrika, Mission 300 itaonyesha dhamira yetu ya pamoja katika kufanikisha upatikanaji wa nishati safi kwa wote, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuboresha maisha ya watu.

"Tanzania inachukulia mkutano huu kama kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati inayolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi. Sera hiyo pia inalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za kisasa za nishati na kuongeza mchango wa nishati mbadala katika mchanganyiko wa uzalishaji ili



kuimarisha upatikanaji, uhakika na usalama wa nishati.

"Ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000. Nishati yetu inatoka kwenye vyanzo safi na mbadala vinavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

"Vile vile, Tanzania inamarisha muunganiko wa Afrika kwani ina miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

"Pamoja na maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati. Tuna matarajio ya kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini, na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

"Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika. Jitihada hizi zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na yamejumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini, huku tukitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

"Miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huu, tutashirikiana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huu.

"Ni matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishati.

"Sasa ni wakati wa kufungua uwezo wa nishati wa bara la Afrika na kukabiliana na pengo la nishati. Tuitumie fursa ya Mkutano huu kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio yetu ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika kuyatekeleza.

Naye Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga katika mkutano huo, aliyasema haya;

"Tunaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030."

Rais wa Benki ya Maendele ya Afrika (AfDB), Dk Akinumwi Adesina alisema: "Tanzania imekua mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

"Nawahakikishia kuwa lengo la kuwafikishia umeme watu milioni 300 Afrika linakwenda kufanikiwa, tunahitaji uwazi na uwajibikaji katika kufikisha lengo hili.

"Mkutano huu una lengo la kuifungua Afrika kwenye eneo la nishati ya umeme, kuhakikisha wananchi katika za Afrika wanaunganishwa na umeme."

# Mapapai yatakavyokupa faida kubwa

NA MWANDISHI WETU

**MAPAPAI ni moja kati ya mazao ya matunda yenye Vitamin A na madini ya 'calcium' kwa wingi na zao hili hulimwa karibu kila mahali hapa nchini kwa wastani wa tani 2,582 kwa mwaka.**

Ili kuweza kuzalisha zao la papai kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa ni muhimu kuhakikisha unazingatia kanuni zote za kilimo bora za uzalishaji wa mapapai. Ubora wa matunda baada ya kuvunwa hutegemea jinsi yalivyozalishwa

Papai bora hutokana na kilimo kilichofuata kanuni sahihi za uzalishaji, hivyo fanya uchaguzi bora wa aina gani za papai katika uzalishaji wako na ni muhimu kuhakikisha unachagua aina iliyobora yenye sifa zinazostahili.

Kwanza unatakiwa uchague aina bora ya kupanda kulingana na uhitaji wa soko na hakikisha aina utakayoichagua inamudu udhibiti wa wadudu, magonjwa pamoja na magugu.

Kumbuka mapapai hushambuliwa kwa urahisi na magonjwa na wadudu hivyo ni muhimu kuhakikisha unafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kugundua dalili za mashambulizi.

Endapo kuna dalili za mashambulizi, dhibiti mapema ili kuzalisha mazao bora yanayoweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu.

Hakikisha shamba na barabra zake ni safi wakati wote ili krahisisha uvunaji pamoja na usafirishaji.

Kingine ni maandalizi kabla ya kuvuna, ambapo unatakiwa kukagua shamba ili kuona kama kuna mapapai yaliyokomaa. Mapapai hukomaa katika kipindi cha miezi mitano kutoka maua yanapochanua.

**Dalili za kukomaa**

Tunda hubadilika rangi kutoka katika ukijani kibichi na kuwa na kijani nyepesi hadi manjano.

**Vifaa kwa ajili ya kuvunia**

Vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kuvuna mapapai ni pamoja na vichumio, mifuko na ngazi.

**Vifaa vya kufungashia**

Ili kufungasha mapapai kwa usahihi vifaa vinavyohitajika ni makasha ya mbao, au plastiki au hata makasha ya makaratasi magumu.

**Vyombo vya kusafirishia**

Mara baada ya kuvuna mapapai ni lazima kusafirisha katika hali yenye ubora kwa kutumia vyombo kama vile mikokoteni, magari pamoja na matela ya matrekta.

**Namna ya kuvuna**

Uvunaji bora wa mapapai ni wa kutumia mikono ambapo tunda huchumwa kwa mkono kwa kutumia kichumio.

Vuna mapapai yaliyokomaa tu na vina papai pamoja na kikonyo chake, vuna kwa uangalifu ili kuepuka kudondosha chini matunda.

Matunda yakidondoka huchubuka, upasuka na hupondeka hivyo husababisha upotevu wa thamani yake na hata kukosa soko, weka mapapai yaliyovunwa kivulini mara tu baada ya kuyavuna.

**Kuchambua**

Ni muhimu kuchambua mapapai ili kutenga yaliyooza, kupasuka na yenye dalili za magonjwa au kubonyea. Lengo la kuchambua ni kupata matunda yenye ubora kulingana na matumizi kwa mfano kusindika, kuuza au kusafirisha.

Matunda yaliyooza na yenye wadudu ni vyema yafukiwe ili kuangamiza wadudu waharibifu na vimelea vya magonjwa na pia kuzuia kuenea kwa wadudu na magonjwa hayo.

Matunda yaliyopasuka, kubonyea au kuchubuka kidogo yatumike haraka kwa kuliwa.

Matunda mazuri ambayo hayatapata madhara yeyote yatumike kwa ajili ya kusindika, kuliwa, kuuzwa au kusafirishwa.

**Kusafisha**

Baada ya kuchambua safisha mapapai kwa maji safi na salama ili kuondoa uchafu wa masalia ya madawa.

Baada ya kusafisha, yatumbukize mapapai kwenye maji ya moto yenye nyuzi joto lipatalo 49 za sentigredi kwa muda wa dakika 20. Maji ya moto husaidia kuua mayai ya viwavi vya wadudu waharibifu wanaoweza kushambulia matunda wakati wa kuhifadhi au kusafirisha.

Muhimu la kuzingatia ni kwamba mapapai hulainika na kubadilika ladha endapo joto la maji litazidi nyuzi 49 za sentigredi zilizoshauriwa.

**Kupanga madaraja**

Madaraja hutakiwa kupangwa kwa lengo la kurahisisha ufungashaji, usafirishaji na uuzaji kwa bei ya juu.

Unatakiwa kupanga madaraja ya mapapai kwa kufuata ubora ambavyo vigezo vyake hutegemea matakwa ya mteja.

Vigezo vya ubora vinavyohitajika ni kama vile ukubwa wa tunda, umbo, rangi, aina na uivaji.

**Kufungasha**

Fungasha mapapai kwenye makasha ili kuzuia yasichubuke, kubonyea au kupasuka wakati wa kusafirisha.

Tandika makaratasi ndani ya makasha ya mbao kabla ya kupanga matunda ili kuzuia kuchubuka kwa matunda.

Hakikisha maksha yana nafasi ya kuruhusu mzunguko wa hewa na kila kasha lisizidi kilo 20 ili kurahisisha ubebaji.

**Kuhifadhi**

Hifadhi mapapai kwenye vyumba vyenye nyuzi joto 10 hadi 20 za sentigredi na unyevu upatao asilimia 85 hadi 95.

Matunda yaliyohifadhiwa katika hali hiyo huweza kudumu kwa muda wa wiki moja bila kuharibika, hasa kama yalikuwa yamekomaa vizuri, kuvunwa vizuri na kutokuwa na michubuko.





# Ngombe wa Kienyeji watakupa faida kiba

NA MWANDISHI MAALUM

**UFUGAJI wa ng'ombe wa kienyeji ni sehemu muhimu sana ya ufugaji na uchumi wa jamii nyingi za Afrika, hasa kwa sababu ya urahisi wake wa kustawisha ng'ombe katika mazingira ya asili na faida zake mbalimbali.**



Ng'ombe wa kienyeji ni wanyama waliobadilika vizuri katika mazingira ya Kiafrika, na wana uwezo wa kuvumilia hali ngumu kama vile ukame, magonjwa, na chakula duni.

Katika blogu hii, tutajadili kwa kina mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji, faida zake, changamoto, na jinsi ya kuzishinda changamoto hizo ili kufanikisha ufugaji wenye tija.

**1. Ng'ombe wa Kienyeji**

Ng'ombe wa kienyeji ni aina ya mifugo ambayo imekuwepo katika mazingira ya Afrika kwa muda mrefu na wamejenga uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimazingira.

Aina hizi za ng'ombe zinapatikana zaidi katika maeneo ya vijijini ambapo wakulima hawana rasilimali nyingi za kuwekeza katika ufugaji wa kisasa.

Ng'ombe hawa hufugwa kwa ajili ya maziwa, nyama, pamoja na bidhaa nyingine kama mbolea ya samadi na ngozi.

**2. Faida za Ufugaji wa Ng'ombe wa Kienyeji**

Ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji una faida nyingi ambazo zinawavutia wafugaji wengi, hasa katika maeneo ya vijijini.

Baadhi ya faida hizo ni: Uvumilivu wa hali mbaya ya hewa, ambapo wana uwezo mkubwa wa kuvumilia hali mbaya ya hewa kama vile joto kali na ukame.

Hii inawafanya wawe chaguo bora katika maeneo yenye mvua kidogo au yenye ukame wa mara kwa mara.

Pia kuna gharama ndogo za matunzo, ikilinganishwa na ng'ombe wa kisasa, ng'ombe wa kienyeji hawahitaji matunzo mengi ya gharama kubwa. Chakula chao kinaweza kuwa nyasi za asili au mabaki ya mazao ambayo hupatikana kwa urahisi mashambani.

**iii. Ustahimilivu wa Magonjwa**

Ng'ombe wa kienyeji kwa Tanzania wana kinga ya asili dhidi ya magonjwa mengi yanayoathiri ng'ombe wa kisasa.

Ingawa wanahitaji uangalizi wa afya kama mifugo mingine, uwezekano wa kuathirika na magonjwa hatari kama homa ya mapafu na homa ya ng'ombe ni mdogo zaidi.

Ubora wa Bidhaa hii ina maana, ng'ombe wa kienyeji hutoa maziwa na nyama zenye virutubisho vya hali ya juu, ingawa uzalishaji wa maziwa ni wa wastani ikilinganishwa na ng'ombe wa kisasa. Pia, nyama ya ng'ombe wa kienyeji inasifika kwa kuwa na ladha bora.

**3. Mbinu Bora za Ufugaji**

Ili kufanikiwa katika ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji, ni muhimu kutumia mbinu bora ambazo zinachangia afya na uzalishaji wa mifugo.

Zifuatazo ni baadhi ya mbinu zinazofaa:

**i. Malisho na Lishe Bora**

Ng'ombe wa kienyeji wanahitaji malisho bora ili kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama.

Malisho haya ni pamoja na nyasi za asili, mikunde, na mabaki ya mazao kama vile majani ya mahindi au pumba za mpunga.

Pia, ni muhimu kuongeza virutubisho kama madini ya calcium na phosphorus ili kuimarisha mifupa na kuongeza uwezo wa uzalishaji.

**ii. Usafi na Mazingira Mazuri**

Mazao ya ng'ombe kama vile maziwa na nyama yanaathiriwa na mazingira ambayo ng'ombe wanafugwa.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa ng'ombe wanakuwa katika mazingira safi, yenye hewa safi na yenye kinga dhidi ya wadudu na magonjwa.

Mabanda ya ng'ombe yanapaswa kuwa na nafasi ya kutosha ili kupunguza msongamano ambao unaweza kusababisha magonjwa.

**iii. Huduma za Afya**

Ingawa ng'ombe wa kienyeji wana kinga ya asili dhidi ya magonjwa, bado ni muhimu kuwa na mpango wa mara kwa mara wa chanjo na tiba za mifugo.

Chanjo dhidi ya magonjwa kama ugonjwa wa miguu na midomo (foot and mouth disease) ni muhimu sana.

Pia, ni muhimu kuangalia afya ya ng'ombe kila mara ili kugundua dalili za magonjwa mapema na kuchukua hatua stahiki.

**iv. Uchaguzi wa Mifugo Bora**

Uzalishaji bora huanza na uchaguzi wa mifugo yenye sifa nzuri.

Wafugaji wanashauriwa kuchagua ng'ombe wenye uwezo mkubwa wa uzalishaji, ambao wana historia ya afya nzuri na wanaweza kuvumilia hali ya kimazingira ya eneo husika.

Uchaguzi huu unaweza kufanywa kupitia ushauri wa wataalamu wa mifugo au wafugaji wenye uzoefu.

**4. Changamoto za Ufugaji wa Ng'ombe wa Kienyeji**

Ingawa ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji una faida nyingi, pia kuna changamoto ambazo zinaweza kuathiri mafanikio ya ufugaji huu.

Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

i. Ukame na Upatikanaji wa Malisho

Ukame ni changamoto kubwa inayowakabili wafugaji wa ng'ombe wa kienyeji, hasa katika maeneo kame na yenye mvua kidogo.

Upatikanaji wa malisho unakuwa mgumu wakati wa kiangazi, na hii inasababisha ng'ombe kudhoofika na kupunguza uzalishaji wa maziwa na nyama.

**ii. Magonjwa ya Mifugo**

Ingawa ng'ombe wa kienyeji wana kinga ya asili dhidi ya magonjwa, bado wanakabiliwa na magonjwa kama vile ndigana kali (East Coast Fever), homa ya mapafu (Contagious Bovine Pleuropneumonia), na minyoo ya tumboni.

Magonjwa haya yanaweza kuathiri afya ya ng'ombe na kupunguza uzalishaji.

**iii. Uwezo Mdogo wa Uzalishaji**

Ng'ombe wa kienyeji kwa kawaida wana uwezo mdogo wa uzalishaji wa maziwa ikilinganishwa na ng'ombe wa kisasa.

Hii inamaanisha kwamba wafugaji wanaweza kupoteza fursa za kiuchumi, hasa wakati wa uhitaji mkubwa wa bidhaa za maziwa.

**5. Jinsi ya Kushinda Changamoto**

Ili kufanikisha ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji licha ya changamoto hizi, kuna hatua kadhaa ambazo wafugaji wanaweza kuchukua:

**i. Kilimo Mseto**

Wafugaji wanaweza kupunguza athari za ukame kwa kutumia mbinu za kilimo mseto ambapo wanafuga ng'ombe pamoja na kilimo cha mazao.

Hii inasaidia kuhakikisha upatikanaji wa malisho ya mifugo hata wakati wa kiangazi.

**ii. Matumizi ya Chanjo na Dawa**

Ili kudhibiti magonjwa, ni muhimu kwa wafugaji kuhakikisha ng'ombe wanapokea chanjo zinazohitajika kwa wakati.

Pia, usimamizi mzuri wa afya kama vile kuzingatia ratiba ya kutoa dawa za minyoo itasaidia kuimarisha afya ya ng'ombe.

**iii. Kuboresha Lishe**

Wafugaji wanashauriwa kuboresha lishe ya ng'ombe wao kwa kuongeza virutubisho vinavyohitajika, hasa wakati wa msimu wa kiangazi ambapo malisho ya asili yanakuwa haba.

**iv. Kuzalisha Mifugo Bora**

Kuchagua mbegu bora za ng'ombe wa kienyeji ambao wana uwezo mkubwa wa uzalishaji na kustahimili mazingira magumu ni njia bora ya kuboresha ufugaji.

Wafugaji wanaweza kuingiza mifugo yenye sifa nzuri za uzalishaji ili kuongeza tija.

**6. Hitimisho**

Ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji unatoa fursa kubwa kwa wafugaji wadogo na wa kati, hasa katika maeneo ya vijijini ambako rasilimali ni chache.

Ingawa kuna changamoto mbalimbali, kwa kutumia mbinu bora za ufugaji kama lishe bora, huduma za afya, na uchaguzi sahihi wa mifugo, inawezekana kufanikisha ufugaji wenye tija.

Ni muhimu kwa wafugaji kuwa na ufahamu wa hali ya soko, mahitaji ya malisho, na huduma za kiafya ili kuhakikisha mifugo inakua na kuzalisha kwa kiwango cha juu zaidi.

# Kuku wa Kienyeji fedha inayotembea



NA MWANDISHI MAALUM

**UFUGAJI wa kuku wa kienyeji ni moja ya shughuli za kiuchumi zinazovutia kutokana na gharama zake ndogo na faida nyingi kwa mfugaji.**

Kuku wa kienyeji ni maarufu sana katika jamii nyingi kutokana na ladha ya nyama yao, mayai yenye ubora wa hali ya juu, na ustahimilivu wa hali ya hewa na magonjwa.

Huu ni ufugaji endelevu unaofaa kwa wakulima wadogo na wa kati.

Kuna muhimu wa kufuga kuku wa kienyeji kwani huchangia kwa usalama wa chakula na hutoa chanzo cha chakula bora chenye virutubisho muhimu kwa familia na jamii.

Pia inatoa ajira na kipato, kwani ufugaji huu huongeza kipato kwa familia na jamii hasa katika maeneo ya vijijini na kuna uhifadhi wa mazingira, ambapo wanahitaji matunzo ya asili yanayosaidia kulinda mazingira.

Ufugaji wa kuku wa kienyeji ni sehemu ya utamaduni wa jamii nyingi, ikihusishwa na sherehe mbalimbali.

Faida za Kuwafuga

Kwanza wana bora ya nyama na mayai, tambua nyama ya kuku wa kienyeji ina ladha nzuri na inayokubalika sana sokoni, huku mayai yao yakiwa na virutubisho vya hali ya juu.

Gharama Ndogo za Matunzo

Kuku wa kienyeji wanaweza kutunzwa kwa kutumia rasilimali za asili kama mabaki ya chakula, nyasi, na wadudu.

Ustahimilivu wa Mazingira

Wanastahimili magonjwa na hali mbaya ya hewa ukilinganisha na kuku wa kisasa. Kuku wa kienyeji huzaliana haraka na kufikia umri wa kuchinjwa au kutaga mayai kwa muda mfupi.

Uzalishaji wa Mifugo Mbadala

Mbali na nyama na mayai, kuku wa kienyeji hutoa mbolea ya asili inayofaa kwa kilimo.

Soko la Uhakika

Kuna mahitaji makubwa ya nyama na mayai ya kuku wa kienyeji sokoni, hasa katika maeneo ya mijini.

Magonjwa

Ingawa wanastahimili magonjwa kwa kiasi, bado wanahitaji chanjo na tiba ya mara kwa mara.

Kiwango Kidogo cha Uzalishaji

Wanazalisha mayai na nyama kwa kiwango kidogo ukilinganisha na kuku wa kisasa.

Ukosefu wa Elimu kwa Wafugaji

Wafugaji wengi hawana ujuzi wa kisasa wa mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Changamoto za Masoko

Ushindani sokoni na ukosefu wa mifumo bora ya masoko huathiri bei ya bidhaa.

Njia za Kukabiliana na Changamoto ni kuhakikisha kuku wanapata chanjo na tiba ya magonjwa kwa wakati. Tumia lishe bora yenye virutubisho vya kutosha kuboresha uzalishaji wa mayai na nyama.

Elimu kwa Wafugaji

Kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji. Kuunda vikundi au ushirika wa wafugaji ili kuongeza ushawishi kwenye soko na kupata bei nzuri.

Mayai na nyama ya kuku wa kienyeji huuzwa kwa bei ya juu sokoni kutokana na ubora wake. Ufugaji huu hauhitaji gharama kubwa za matunzo.

Ufugaji wa kuku wa kienyeji unasaidia kuboresha maisha ya jamii kwa kuongeza kipato na chakula bora. Mbolea inayotokana na kuku wa kienyeji husaidia kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Ufugaji wa kuku wa kienyeji ni fursa nzuri kwa wakulima wadogo na wa kati wanaotafuta njia endelevu ya kuongeza kipato na kuboresha maisha yao.

Kwa gharama nafuu, nyama na mayai yenye ubora wa hali ya juu, na ustahimilivu wa mazingira, ufugaji huu unafaa kuimarishwa kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo na mifugo.

Kwa kutumia mbinu bora na kushughulikia changamoto zilizopo, faida kubwa inaweza kupatikana kutoka kwenye ufugaji huu endelevu.



# Umehaha kusaka fedha? Huku usiende

NA MWANDISHI MAALUM

**DUNIA imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya kuvutia, ambayo hukusanya watu wa mataifa mbalimbali kuyatembelea. Kawaida vivutio vingi vinawekewa utaratibu ukiwemo wa utunzaji na malipo.**

Mwaka 2019, sekta ya utalii duniani ilichangia asilimia 10.4% ya pato ghafi la dunia. Lakini yapo maeneo mazuri yangeweza kuchangia zaidi, ila ni marufuku kukanyaga.

Mamilioni ya watalii hutembelea hifadhi za wanyamapori, milima mirefu, majumba ya kale, maeneo ya utamaduni na maeneo mengine yanayowavutia.

Lakini yapo maeneo duniani ambayo watalii wangetamani kutembelea lakini kwa sababu ya sifa zake na historia yake yanaleta kikwazo. Mengi yamekuwepo bila kutunzwa kitalii lakini yanavutia kwa historia yake na vilivyomo.

Mengine ni wanasayansi tu huruhusiwa kuyafikia kwa masharti maalumu, maeneo mengine wala hukatazwi kuyatembelea lakini yanahitaji moyo wa kipekee kuyatembelea.

Kwa wenye imani, wengine wanasema kuwepo kwa maeneo ya aina hiyo kunaonesha ukuu wa uumbaji wa Mungu.

Ingawa yapo maeneo zaidi ya 30 yenye sifa hizi, lakini BBC inakuletea orodha ya maeneo sita ambayo watalii mwiko kuyatembelea licha ya uzuri na historia ya kuvutia ya maeneo hayo.

**1. Mapango ya Lascaux, Ufaransa**

Haya ni mapango marefu yanayopatikana kaskazini mashariki mwa Ufaransa. Ni moja ya mapango ambayo kunapatikana michoro mizuri na maarufu zaidi ya kihistoria duniani. Inaelezwa ni michoro ya siku nyingi ya enzi za mababu wa mababu ikitajwa kuwa ina miaka zaidi ya 17,000.

Michoro mingi ni ya wanayama wakubwa wakubwa ambao wanatajwa waliishi miaka hiyo katika maeneo hayo. Mapango hayo yameorodheshwa na kutambulika na Shirika la Umoja wa Mataifa la elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kama urithi wa dunia.

Nyumba ni bure na ni nzuri ,lakini hakuna anayetaka kuishi katika paradiso hii,kunani?

Hata hivyo mapango hayo yamefungwa kutokana na mlipuko wa fangasi wanaotoko kwenye mapango hayo. Wakiruhusiwa wasayansi wachache sana angalau mara moja moja kwa mwezi kwa lengo la kutafiti.

**2. Kisiwa cha North Sentinel, India**

Ni kisiwa kidogo sana chenye msitu mnene zaidi kwenye ghuba ya Bengal. Ni moja ya visiwa vya Andaman kwenye bahari ya Hindi, kilichozungukwa na miamba mikubwa ya mawe ya matumbawe, hali inayoleta ugumu kukifikia kwa njia ya boti.

Lakini hicho sio kikwazo pekee cha watu kutoruhusiwa kufika ama kushindwa kutembelea, kikwazo kikubwa ni kwamba kisiwa hicho ni makazi ya watu wa jamii ya Sentinel ambao hawataki muingiliano na watu wengine duniani.

Inaelezwa ndio jamii iliyosalia duniani ambayo haijaguswa na maisha ya kileo na dunia ya sasa.

Mwaka 2008, wavuvi wawili ambao boti yao kwa bahati mbaya ilikaribia kisiwa hicho waliuawa na watu hao. Na mwaka 2004 wakati wa dhoruba kubwa la Sunami, wanasayansi walitumia helkopta kuangalia athari zilizowakumba watu hao. Wakiwa kwenye anga za fukwe walianza kushambuliwa kwa mishale, mikuki na mawe.

3. Doomsday Vault, Norway

The Doomsday Vault ni benki ama ghala kubwa la mbegu duniani, linalopatikana nchini Norway. Kila mbegu unayoijua duniani na kutumika kwenye kupata zao inahifadhiwa hapo.

Ghala hili liko mbali na makazi ya watu na mahala ambapo hata vita ikitokea ama gharika lolote likitokea mbegu hizo zitaendelea kuwa salama.

Sehemu kubwa ya ghala hilo iko ardhini na haifikiki kirahisi labda kwa watumishi wachache wanaofanya kazi hapo. Ni eneo lenye baridi sana na kulindwa wakati wote.

**4. Poveglia, Italia**

Kisiwa kingine kidogo kinachopatikana kati ya Venice na Lido kaskazini mwa Italia. Katika historia ya kisiwa hicho, ni mahala panapopatikana sana ngome kongwe , mahala ambapo palitumika kama kituo cha kuangalia usalama wa meli na baadaye pakatumika kama karantini ya kuwahifadhi wagonjwa wenye magonjwa mbalimbali hasa ya mlipuko na magojwa ya akili.

Lakini mwaka 1968, hospitali iliyokuwa inatumika kwa wagonjwa hao ambao wengi walikuwa wenye magojwa ya akili, ilifungwa na tangu wakati huo, kisiwa hicho kimetelekezwa.

Kuna hisia kwamba tangu kufungwa kwa hospital hiyo, mizimu ya wagonjwa waliofariki, watu waliouawa kweye vita inaendelea kuwepo kwenye majengo ya kisiwa hicho. Kumedaiwa kuwepo kwa sauti zikisikika kwenye miamba na mawe yaliyoporomoka.

Sauti zisizoeleweka. Watu wengi walikacha kwenda kwa hofu. Mwaka 2014 Serikali ya Italia iliwahi kutangaza kukipangisha kisiwa hicho kwa miaka 99 ili kuvutia watu watakaokiendeleza, lakini hofu imetawala zaidi ya kufika huko.

**5: Kisiwa cha Nyoka, Brazil**

Kama jina lake lilivyo, Kisiwa cha nyoka chini Brazil (Ilha da Queimada Grande) ni eneo lenye nyoka wengi na wakali pengine kuliko maeneo yote duniani yenye ukubwa huo.


Ni eneo lenye ukubwa wa hekari 43 na nyoka wanaopatikana wanatajwa kuwa na sumu kali zaidi na inayoweza kuua binadamu kwa haraka.

Kila mita za mraba tano kuna nyoka, ni sawa na hatua kama tano ukitembea kwa miguu lazima ukutane na nyoka wa ukubwa tofauti.

Utafiti unaonesha kuna nyota zaidi ya 4,000 aina ya Golden Lancehead Viper wanaopatikana kwenye kisiwa hicho kilichoko maili takribani 20 kutoka pwani ya mji wa Sao Paulo.

Serikali ya nchi hiyo imepiga marufu binadamu yeyote kutembelea kisiwa hicho kwa sababu ya usalama.

Wanasayansi wachache tena kwa tahadhari kubwa na nyenzo za kisasa za kujilinda wamekuwa wakiruhusiwa kufanya utafiti kila baada ya miaka mitano tena kwa vibali maalumu vya kufa ama kupona.





# DAVIDO

## ATAJA UTAJIRI WA BABA YAKE

LAGOS, Nigeria

**SUPASTAA wa muziki wa Nigeria, Davido, ameweka wazi kuwa fedha za baba yake hazijawahi kumsaidia kupata mafanikio aliyonayo kwenye sanaa.**

**Davido, katika mahojiano yake ya hivi karibuni, alisema baba yake ni tajiri lakini alitaka watoto wake waishi maisha ya kawaida. "Ilinichukua miaka mingi kujua kama baba yangu ni tajiri," alisema Davido ambaye ni mmoja ya wasanii matajiri Afrika.**

## KUMBE RAPA HUYU ALITAKA KUUAWA

LAGOS, Nigeria

**RAPA wa Nigeria anayeishi Marekani, Yung6ix, ameeleza alivyonusurika kifo katika tukio la kuvamiwa na wahuni jijini Los Angeles.**

Akisimulia tukio hilo, alisema wezi hao walimrushia risasi wakati akiwa kwenye gari lake lakini zilimkosa. Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram, alisema dua za mama yake ndizo zilizomsaidia.

## BURNA BOY APEWA FAGIO LAKE




MANCHESTER, City

MCHEZAJI mpya wa Manchester City, Omar Marmoush, amekiri kuvutiwa na mwanamuziki wa Nigeria, Burna Boy.

Mshambuliaji huyo raia wa Misri amejiunga na Man City akitokea Bundesliga alikokuwa akiitumikia Eintracht Frankfurt.

Wakati huo huo, Marmoush aliweka wazi kuwa Ronaldinho ndiye mchezaji aliyemvutia zaidi tangu akiwa mdogo.





# KITANZI

## CHAMRUKA BOSI CAF

CAIRO, Misri

**SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF) limetangaza kuwa Katibu Mkuu wake, Veron Mosengo-Omba, hatafunguliwa mashitaka ya rushwa.**

CAF wameibuka baada ya kigogo huyo kutumuhiwa kwa vitendo vya rushwa na waendesha mashitaka wa Uswis.

Mosengo-Omba, raia wa Uswis mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), anatajwa kujichotea fedha za CAF.

## MBAPPE AAMUA KUNENA



MADRID, Hispania

**SUPASTAA wa Real Madrid, Kylian Mbappe, amesema kwake kufunga mabao siyo jambo la msingi na badala yake anataka kuona timu hiyo ikitwaa mataji.**

Mbappe ameibuka na kauli hiyo baada ya kupachika 'hat trick' katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Real Valladolid, mchezo wa La Liga uliochezwa wikiendi iliyopita.

## BARCELONA WASHIKANA MASHATI

CATALUNYA, Hispania

**KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, amewataka wachezaji wake kujitafakari baada ya sare ya bao 1-1 waliyoipata wikiendi iliyopita dhidi ya Getafe.**

Tangu walipoifunga Real Madrid katika mchezo wa Spanish Super Cup, Barca wamekuwa na mwenendo mbovu, ikiwa ni pamoja na kushinda mechi moja tu tangu Desemba, mwaka jana. "Tumedondosha pointi nyingi kwenye Ligi. Kilichotokea dhidi ya Getafe ni makosa yetu. Hatukuwa na umakini wa kutosha," alisema.

## MOTTA RATIBA YAMBANA




TURIN, Italia

**KOCHA wa Juventus, Thiago Motta, ameutaja ugumu wa ratiba ndiyo sababu ya timu yake kupoteza mchezo uliopita dhidi ya Napoli.**

Kwa mujibu wa Motta, Napoli walikuwa na wiki nzima ya mapumziko wakati wao walikuwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.
"Tumetoka kucheza mechi nyingi na ilikuwa wazi katika kipindi cha pili, ambapo tulionekana tumechoka kabisa," alisema kiungo huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Italia.

Mjasiriamali spoti

MJASIRIAMALI JANUARI 28, 2025

Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# SIMBA: HUYU FADLU NOMA

NA ELLY SARONGO

**PONGEZI KWAKE! Simba imempongeza kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids na kusema, alichofanya katika mchezo wa juzi dhidi ya Kilimanjaro Wonderers alifanya kitu kizuri zaidi kwa kuwaamini wachezaji wake.**

Juzi, Simba ilikutana na Kilimanjaro Wonderers katika mchezo wa Kombe la Shirikisho la TFF, uliopigwa katika Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salam ambapo iliondoka na ushindi wa mabao 6-0 na kufanikiwa kuingia Raundi ya 32 Bora.

Akizungumza mara baada ya mchedzo huo, Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally alisema Fadlu amefanya kitu kizuri kwa kuwaamini wachezaji wake na kuwapa nafasi ya kucheza katika mchezo huo.

"Kwanza napenda kumpongeza Fadlu kwa kuwaamini wachezaji wake wote na kuwapa nafasi katika mchezo huu, pia huu ulikuwa mchezo muhimu kwa mashabiki ambao walikuja kuwapa shukrani wachezaji wao.

"Unajua timu imecheza mechi tatu na mashabiki hawakupata fursa ya kuwaona wachezaji wao, tulicheza Tunisia, Angola tukaja mechi ya Dar es Salaam na mechi zote tatu hizi hatukuwaona wachezaji wetu.

"Tunisia hatukuwepo, Angola hatukuwepo na Dar es Salaam tulikuwa tumekula ubaya ubwela, hivyo mashabiki walikuja ili kuwapongeza wachezaji wao kwa kazi kubwa waliyofanya."

## MZIZE ANATISHA KWA REKODI

NA MWANDISHI WETU

**Hazungumzwi sana, lakini rekodi alizonazo ndani ya kikosi cha Yanga zinambeba, Clement Mzize aliyegeuka kuwa mshambuliaji hatari na muhimu wa kikosi hicho kilichopo chini ya kocha Sead Ramovic.**

Mshambuliaji huyo mzawa licha ya kuletewa mastaa wengi wa kigeni ndani ya timu hiyo, bado ameonekana kuuwasha na kubeba rekodi nzuri kuliko mastaa hao anaocheza nao nafasi moja Jangwani.

Akiwa na msimu wa tatu tangu alipopandishwa akitokea timu ya vijana, Mzize amezidi kuwa mtamu akimfunika hadi Kennedy Musonda anayelingana muda wa kuitumikia timu hiyo, akipita mikononi mwa makocha Nasreddine Nabi na Miguel Gamondi kabla ya kuja kwa Sead Ramovic.



Katika misimu mitatu ya Ligi rekodi zinaonyesha Mzize amemkimbiza Musonda ambaye amekuwa akiimbwa kwenye kikosi hicho, kwani amehusika katika mabao 25 (kabla ya mechi dhidi ya Fountain Gate FC), akifunga mabao 16 na asisti tisa, wakati Musonda akifunga jumla ya mabao 11 na asisti mbili ndani ya misimu hiyo mitatu kwa Ligi Kuu.

Katika msimu wa Mzize wa kwanza wa 2022/23 alikuwa sehemu ya kikosi kilichoipa timu hiyo taji la Ligi Kuu akifunga mabao matano na kutoa pasi moja iliyozaa bao, hivyo alihusika kwenye mabao sita kati ya mabao 43 yaliyofungwa na timu hiyo huku Fiston Mayele (Yanga) na Saidoo Ntibanzonkiza (Simba) wakiibuka wafungaji bora baada ya kupachika mabao 17 kila mmoja.

Kwa Musonda rekodi zinaonyesha msimu huo akiingia katika dirisha dogo, alifunga mabao manne bila ya asisti, ilihali katika msimu wao wa pili, Mzize alifunga mabao sita na kuasisti saba, akimuacha mbali Mzambia huyo aliyefunga mabao matano na asisti mbili.

